

# MIAKA HAMSINI YA KISWAHILI NCHINI KENYA



**WAHARIRI:** Inyani Simala | Leonard Chacha | Miriam Osore

SURA YA SITA

# UFUNDISHAJI WA KISWAHILI KATIKA NCHI ZA KIGENI: MFANO WA CHUO KIKUU CHA SYRACUSE

Miriam Osore na Brenda Midika

## Utangulizi

Ufundishaji na ujifunzaji wa lugha za Kiafrika katika nchi za kigeni unahitaji historia ndefu. Kwa mujibu wa Moshi katika Bokamba (2000: uk 26-27) ufundishaji wa lugha za Kiafrika haukuanzia madarasani bali ulianzishwa nyanjani katika karne ya 15 ambapo wamishenari walitaka kujua zaidi kuhusu lugha za jamii walizokuwa wakienyeza injili. Walianza kwa kuandika makamusi na vitabu vya sarufi ambavyo viliwahamasisha wanaisimu kamwe vile Wilhelm Bleek ambaye alichapisha kitabu *A Comparative Grammar of African Languages*. Miongoni mwa wanaisimu wengine ni kama Jame Frederick Schon na Carl Meinhof ambaye alichapisha kitabu cha fonolojia ya lugha za Kibantu na Johann Ludwig Krapf aliyechapisha kitabu cha kwanza cha sarufi ya Kiswahili.

Mafunzo ya lugha za Kiafrika nchini Marekani yalianzishwa miaka ya 1950, kama kipengele muhimu cha sheria ya Taifa, *The National Defense Act* ya 1958, Sheria hii ilianzisha vituo vya mafunzo kuhusu Afrika. Mafunzo haya yalikusishwa hasa lugha na fasihi. Kuanzia wakati huo vyuo nchini Marekani vimekuwa vikifunza lugha za Kiafrika ikiwemo lugha ya Kiswahili. Katika kuadhimisha miaka 50 ya Kiswahili ni muhimu kutathmini namna taaluma ya ufundishaji wa Kiswahili katika nchini za Kigeni inavyoendelea na mchango wake katika maenezi ya Kiswahili kimataifa. Makala hii yanalenga kufafanua ufundishaji wa lugha ya Kiswahili nchini Marekani. Yanagusia mbinu za ufundishaji kama, matumizi ya teknolojia na changamoto ambazo walimu Waafrika wanakumbana nazo katika kufundisha wazungu Kiswahili hasa katika Chuo Kikuu cha Syracuse.

## Historia ya ufundishaji wa lugha za Kiafrika Marekani

Kama ilivyotajwa, mpango wa kufundisha lugha za Kiafrika Marekani una historia ndefu. Moshi (2011) anaeleza kuwa utekelezaji wa sheria ya Taifa ya *The National Defense Act* ya mwaka wa 1958 ulikuwa chanzo cha mabadiliko ya mitazamo kuhusu Lugha za Kiafrika huko Marekani. Kutokana na hatua hiyo, taaluma ya Lugha za Kiafrika ilipiga hatua kubwa kuanzia mwaka 1999. Hata hivyo, ufundishaji wa Lugha za Kiafrika umepitia changamoto nyingi kwa mfano, mbinu zinazotumiwa kufundisha, uteuzi wa lugha zitakazofunzwa, ufadhili wa programu zinazolenga Lugha za Kiafrika na kutokuwepo kwa wanafunzi wa kutosha. Baadhi ya changamoto hizi zimeweza kukabiliwa kupitia juhudi za ushirikiano baina ya walimu wa lugha hizi na washikadau wa sekta ya lugha za Kiafrika kama vile watafiti na wanafunzi wa shahada za juu.

Sheria ya Taifa ya *The National Defense Act* ya mwaka wa 1958, iliidhinisha masomo ya lugha za Kiafrika kuanzishwa katika vyuo na vituo maalumu vilivyochaguliwa ili kutimiza malengo ya sheria hii. Hii ilitokana na utetezi wa haki za watu weusi ambao walitaka kujitambulisha na bara la Afrika na lugha za Afrika. Waafrika hawa walitaka kujihusisha na Afrika pamoja na mila, desturi na utamaduni wake. Kutokana na mwamko huu wanafunzi wengi wenye asili ya Afrika (Waafrika Weusi) walidai mafunzo ya lugha za Kiafrika yatolewe katika mitaala yao. Haya yalitendeka katika miaka ya 1960 (Temu, 1992). Waafrika wengi walikuwa wamesikia kuhusu utamaduni wa bara la Afrika ambalo lilikuwa asili yao. Temu (1992) anaeleza kuwa ili kuweza kujihusisha zaidi na kujifahamisha vilivyo kuhusu Afrika, vyuo vililazimika kutoa mafunzo ya lugha na tamaduni za Kiafrika. Miongoni mwa lugha ambazo zilipendekezwa zilikuwa Kiswahili, Hausa, Yoruba na Kiigbo. Temu (1992) anafafanua zaidi kuwa kufikia miaka ya 1960, lugha za Kiafrika hazikuwa zimepewa umaarufu sana. Hata hivyo, Kiswahili ndicho kilipewa umaarufu zaidi ya lugha nyingine na ndicho kilikuwa lugha yenye idadi kubwa ya wanafunzi.

Kufikia miaka ya 1970 lugha za Kiafrika zilikuwa zinaendelea kupata umaarufu katika vyuo kadhaa. Wiley (2008) anaeleza kuwa kuanzia mwaka wa 1972 kulikuwa na ushirikiano baina ya wasimamizi wa mipango ya masomo ya Kiafrika, walimu na wapenzi wa lugha za Kiafrika. Kongamano la kila mwaka la Isimu ya Lugha za Kiafrika lililoanzishwa mwaka wa 1970 liliwaleta pamoja walimu wa lugha za Kiafrika kwa ajili ya kubadilishana maoni kuhusu ufundishaji na ujifunzaji wa lugha za Kiafrika. Hata hivyo,

kongamano hili halikuzingatia sana maswala ya ufundishaji wa lugha za Kiafrika bali lilijikita zaidi katika isimu ya lugha za Kiafrika (Moshi, 2011). Kutokana na mikutano ya walimu wa lugha za Kiafrika katika kongamano hili, *Chama cha Walimu wa Lugha za Kiafrika* kilianzishwa. Chama hiki kilitokana na kubaguliwa kwa lugha za Kiafrika nchini Marekani (Moshi, 2011). Sababu nyingine ya uundaji wa chama hiki ilikuwa ni kushughulikia hali ya ufundishaji wa lugha za Kiafrika hasa mbinu za ufundishaji na vifaa vya kufundishia. Walimu hawa walikutana katika vyuo kadhaa kujadili njia na mbinu za kuboresha ufundishaji wa lugha za Kiafrika (Moshi 2011).

Miaka ya 1980 ilishuhudia kukua kwa taaluma ya lugha za Kiafrika. *Kituo cha Kitaifa cha Lugha za Kiafrika (National African Resource Centre)* kilianzishwa mwaka wa 1988. Kituo hiki kimekuwa na jukumu kubwa la kusambaza vifaa vya kufundishia lugha za Kiafrika miongoni mwa walimu wa lugha hizo. Juhudi za *Baraza la Kitaifa la Mashirika Yanayoshughulikia Lugha Zisizofunzwa sana Nchini (National Council of Organizations of Less Commonly Taught Languages, NCOLCTL)*, na ushirikiano wa walimu wanaofunza lugha hizi umechangia zaidi katika kukua kwa taaluma ya ufundishaji wa lugha za Kiafrika. Taaluma ya lugha za Kiafrika imeendelea kukua na kwa sasa lugha hizi zinaendelea kupata ongezeko la idadi ya wanafunzi. Wiley (2008) anaeleza kuwa katika mwaka wa 2001-2002 wanafunzi 1500 walijisajili kwa masomo ya lugha za Kiafrika katika vyuo vya Marekani huku 139 wakifadhiliwa kwa masomo zaidi katika lugha za Kiafrika. Kama ilivyokwisha kueleza hapo juu, Kiswahili ndiyo lugha ya Kiafrika inayofunzwa nchini Marekani na yenye umaarufu zaidi. Wiley (2008) anasema kuwa taasisi za elimu 106 nchini Marekani hutoa masomo ya Kiswahili huku 32 zikitoa masomo ya lugha ya Kiyoruba, 16 ya Kiwolofu na 8 ya Kihausa.

Vyuo vingi vya Marekani hutegemea wanafunzi au walimu kutoka Bara la Afrika kuja kufunza masomo ya lugha hizi za Kiafrika chini ya wasimamizi wa programu za lugha hizi. Walimu hawa huwa wanafunzi wa masomo mengine, hasa fasihi ya Kiafrika na isimu ya lugha za Kibantu. Moshi (2011) anafafanua kuwa hali ya kushirikisha nyanja hizi mbili na ufundishaji wa lugha za Kiafrika ndiyo imekuwa msingi mkuu wa kuzishikilia lugha za Kiafrika katika nafasi ifaayo. Hali hii imewezesha walimu hawa kufadhiliwa kimasomo. Kwa upande mwingine, juhudi za serikali ya Marekani katika kutambulisha Kiswahili kama mojawapo ya lugha muhimu zimewezesha Kiswahili kupata ufadhili zaidi. Maelezo haya yanadhihirisha kuwa kwa

zaidi ya miaka 50, lugha ya Kiswahili imeendelea kupata umaarufu na kuenezwa zaidi Marekani.

Hali ya ukuaji wa ufundishaji na ujifunzaji wa lugha za Kiafrika nchini Marekani imepata changamoto si haba katika miaka ya hivi karibuni. Ufadhili wa miradi ya ufundishaji wa Kiswahili ulipunguka katika miaka ya 2008-2011 kutokana na mfumuko wa uchumi ulimwenguni. Upungufu wa ufadhili uliathiri masomo katika vyuo kadhaa. Ingawa vyuo vingi vya kibinafsi viliathiriwa sana na upungufu huu, viliendelea kutoa masomo ya lugha ya Kiswahili. Chuo Kikuu cha Syracuse ni mojawapo ya vyuo vya kibinafsi nchini Marekani vilivyoendelea kutoa masomo ya lugha ya Kiswahili.

### **Historia ya ufundishaji wa Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Syracuse**

Lugha ya Kiswahili ndiyo lugha ya pekee ya Kiafrika inayofundishwa katika Chuo Kikuu cha Syracuse. Masomo ya Kiswahili yalianzishwa mwaka wa 1972 katika Mpango wa Masomo ya Kiafrika. Masomo haya yalifundishwa hadi mwaka wa 1980. Katika mwaka huo, ufadhili wake ulipunguka na hivyo basi masomo yakasitishwa. Mnamo miaka ya 1990 hakukuwepo na masomo ya Kiswahili na kufikia miaka ya awali ya 2000 masomo ya Kiswahili hayakuwa yamerejeshwa.

Katika mwaka wa 2005 Idara ya Lugha, Fasihi na Isimu katika Chuo hiki ilichukua jukumu la kufufua masomo ya Kiswahili huku ikitegemea walimu wa Kiswahili kutoka kwa Shirika la Fulbright. Walimu hawa wanafadhiliwa na mradi wa *Fulbright Foreign Language Teaching Assistantship - FLTA*. Masomo ya Kiswahili yameendelea kukuja katika Chuo cha Syracuse chini ya mradi huu wa Fulbright. Mwanafunzi anatarajiwa kumaliza kozi nzima ya Kiswahili ikiwa ni SWA 101- *Beginner Swahili*, SWA 102 na SWA 201- *Intermediate Swahili*, na SWA 202- *Advanced Swahili*. Wanafunzi wa Chuo kutoka idara mbalimbali huruhusiwa kuchukua masomo ya Kiswahili hata kama hawajajisajili au kulipia mojawapo ya kozi hizi. Madarasa hujumuisha wanafunzi wa isimu, uhandisi, masomo ya uhusiano wa kimataifa, biashara, historia, habari na mawasiliano na kadhalika. Mara nyingi darasa huwa na wanafunzi ambao hawajajisajili katika mifumo ya vyuo lakini wana ruhusa kutoka kwa msisimazi wa idara ya Lugha, Fasihi na Isimu. Idadi hii ya wanafunzi imeendelea kuongezeka zaidi na kufikia mwanzo wa muhula wa masomo wa 2013/2014 wanafunzi waliotaka kujifunza SWA 101 walikuwa takribani 13. Kiwango hiki kinaonyesha ukuaji katika masomo ya Kiswahili katika Chuo hiki.

Katika mwaka wa masomo wa 2013/2014 Chuo Kikuu cha Syracuse hakitaweza kutoa masomo ya Kiswahili kutokana na changamoto zisizoepukika. Kwanza, wanafunzi wanaotaka kujifunza Kiswahili wameongezeka lakini wanafunzi wanaolipia kozi hii sio wengi sana. Vyuo vingi nchini Marekani hutoa masomo mengi huku vikizingatia viwango vya wanafunzi waliojisajili na kulipia kozi. Katika Chuo hiki wanafunzi wenye haja ya kukisoma Kiswahili ni wengi ilhali wale waliojisajili walikuwa 3 pekee. Hivyo basi, idadi hii ndogo ya wanafunzi waliojisajili iliathiri masomo ya Kiswahili. Pigo kubwa zaidi kwa masomo ya Kiswahili ni kuwa Chuo Kikuu cha Syracuse hakikuweza kupata mwalimu wa Kiswahili chini ya mradi wa Fulbright. Kutokana na mfumuko wa uchumi ulimwenguni, Serikali ya Marekani imekuwa ikipunguza viwango vya ufadhili wa miradi mingine ikiwemo mradi wa Fulbright.

Hata hivyo, kuna matumaini kwa kuwa Idara ya Masomo ya Kiafrika inaazimia kuhamisha somo la Kiswahili kutoka Idara ya Lugha, Fasihi na Isimu. Katika Idara hii wapenzi wa masomo ya Kiafrika wanatia bidii zaidi katika kutafuta mbinu nyingine za ufadhili ili kuendelea kukidhi mahitaji ya idadi kubwa ya wanafunzi wanaotaka kujifunza Kiswahili. Kwa upande mwingine vyuo na mashirika kadhaa yameanza kuongeza ufadhili wao kwa miradi ya masomo ya Kiafrika na kwamba Chuo Kikuu cha Syracuse katika miaka ijayo kitaweza kupata ufadhili wa kulisimua masomo ya Kiswahili.

Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Syracuse kimepata umaarufu sio tu kutokana na ufadhili wake bali pia kutokana na walimu wenye asili ya Kiafrika wanaofahamu utamaduni na historia ya Afrika Mashariki. Walimu hawa pia wana weledi wa lugha na tajriba ya kuwa katika mazingira halisi ya Kiafrika. Baadhi ya wanafunzi wameeleza kuwa sababu mojawapo ya kusoma Kiswahili ni kutaka kutembelea Bara la Afrika hasa Afrika Mashariki. Lakini siyo tu ule weledi wa lugha ambao utalifanya somo la Kiswahili kufurahisha katika Chuo hiki bali ni kuweza kuelewa utamaduni wa wanafunzi hawa na mbinu za kuweza kuwachangamsha kila siku ili waweze kuja darasani.

Mojawapo ya itikadi ya jamii zilizoendelea ni matumizi ya teknolojia. Hivyo basi, mwalimu kutoka Bara la Afrika lazima ajifunze namna ya kuhusisha teknolojia katika ufundishaji wake. Chuo Kikuu cha Syracuse kimewasisitizia walimu wa lugha kutumia teknolojia katika ufundishaji. Kunayo semina baada ya kila wiki tatu ya kuwafunza walimu mbinu mpya za teknolojia na ufundishaji wa lugha inayoandaliwa na Idara ya Lugha,

Fasihi na Isimu na Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na Huduma Nyingine. Semina hizi zimewasaidia sana walimu wa lugha katika kuhusisha teknolojia katika ufundishaji wa lugha. Lugha ya Kiswahili pia imenufaika na semina hizi. Teknolojia katika nchi zilizoendelea huathiri mno masomo na katika miaka ya hivi karibuni, suala kubwa katika ufundishaji wa lugha ni utumiaji wa teknolojia katika ufundishaji lugha utakaomnufaisha mwalimu na mwanafunzi.

### **Teknolojia, ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili**

Teknolojia ni njia kuu ambayo inaweza kuathiri ufundishaji wa lugha ya pili au lugha ya kigeni. Katika nchi zilizoendelea, teknolojia ni nyenzo kuu katika ufundishaji. Ufundishaji kwa kutumia teknolojia hutegemea vifaa vya kiteknolojia katika kukidhi malengo ya mwalimu ya kuwasilisha hoja na mafunzo kwa wanafunzi. Ufundishaji wa lugha za pili au za kigeni na matumizi ya Kompyuta (*Computer Assisted Language learning*) ni vifaa ambavyo hutiliwa maanani sana. Hoopingarner (2009) anaeleza kuwa mbinu nzuri zaidi katika kutumia teknolojia ili kusaidi katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha, ni mbinu ambayo huona teknolojia kama kifaa cha kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji wa lugha. Mbinu hii huona teknolojia kama kifaa cha kuisisimua mafunzo na kutoa fursa zaidi za kufanya mazoezi ya lugha. Pia mbinu hii huchukulia teknolojia kama jukwaa la kutangamana na kutoa majukumu yaliyo na mwelekeo wa kumnufaisha mwalimu na mwanafunzi.

Blake (2008) katika *A Brave New Digital Classroom: Technology and Foreign Language Teaching* anafafanua mbinu za kumsaidia mwalimu mgeni anayebadilisha mazingira yake na kujikuta katika mazingira ya nchi iliyoendelea. Mwalimu huyu anatarajiwa kufunza lugha ya kigeni akitumia teknolojia. Blake anafafanua mambo manne ambayo ni kinyume na matumizi ya teknolojia. Mambo haya huathiri mwelekeo wa mwalimu mgeni katika ufundishaji wake wa lugha ya kigeni. Mambo haya yanajumuisha:

- (i) Lazima mwalimu afahamu kuwa *teknolojia pekee haiwezi kutimiza mahitaji ya ufundishaji wa lugha* bali ujumuishaji wa teknolojia na mbinu zingine za ufundishaji ni jambo msingi katika matumizi ya teknolojia katika ufundishaji wa lugha.
- (ii) Teknolojia ni tofauti na mbinu zingine za ufundishaji ambazo *hujikita katika misingi ya kinadharia*. Teknolojia haijikiti katika misingi yoyote

ya kinadharia, ni jukumu la mwalimu kujiwekea misingi yake katika matumizi ya teknolojia katika kufundisha lugha. Mwalimu ana jukumu la kuweka misingi yake katika kuunda itikadi yake ya matumizi ya teknolojia na ufundishaji wa lugha.

- (iii) Sio tu teknolojia ya *kisasa ambayo tunahitaji kujua bali pia teknolojia ya hapo awali*. Teknolojia hubadilika na sio tu kuwa teknolojia hubaki pale pale. Ingawa teknolojia inabadilika ni muhimu kufahamu namna ya kujumuisha teknolojia ya awali na teknolojia ya kisasa.
- (iv) Teknolojia *haiwezi kuchukua nafasi ya mwalimu*. Mwalimu ni msaidizi tu katika matumizi ya teknolojia na kwamba lazima teknolojia itumike katika kufanikisha masomo na sio katika kuchukua nafasi ya mwalimu.

Cetto (2011) anaeleza kuwa la msingi ni kukumbuka kwamba teknolojia yaweza kuboresha kiwango cha ufundishaji wa lugha na kuwezesha kiwango cha mwalimu katika kufunza lugha. Katika miaka ijayo, ufundishaji wa lugha za Kiafrika utaathiriwa sana na teknolojia. Mugane (1997) anafafanua kuwa teknolojia inatoa fursa ya kuboresha ufundishaji wa lugha za Kiafrika na kwamba utenganishaji wa lugha na teknolojia hautanufaisha ufundishaji na ujifunzaji wa lugha za Kiafrika. Mwalimu na mwanafunzi wanaweza kunufaika zaidi na matumizi ya teknolojia katika kujifunza lugha kutokana na fursa nyingi ambazo teknolojia hutoa ili kuboresha sio tu matamshi, bali utangamano wa lugha inayofunzwa na mandhari halisi ya lugha hiyo. Miongoni mwa teknolojia ambayo inatumika chuoni Syracuse kuboresha ufundishaji wa Kiswahili ni kama vile YouTube, Google Docs, mitandao ya kijamii, mtandao, video na CD. Mambo hayo yamefafanuliwa hapa chini.

## **YouTube**

*YouTube* ni aina ya teknolojia inayopatikana mtandaoni na hutumia video ambazo zinasambazwa kwa umma. Mtu yeyote anaweza kutazama video za Youtube. Snelson (2008) anaeleza kuwa video ina thamani kubwa kama kiwasilisha cha picha ambacho huleta uhalisia katika ubongo wa mwanafunzi. Video humwezesha mwalimu kuonyesha maeneo ya mbali, historia ya jamii, wanyama, hadithi za digitali na mengi zaidi. Mwanafunzi huweza kuhuisa masomo kupitia kutazama mazingira ya pwani mwa Kenya, maisha mjini Nairobi, maisha katika sehemu za bara na mazingira tofauti. Kupitia *YouTube* mwalimu huwapa wanafunzi mazoezi kama vile

kutafuta wimbo wa Kiswahili ambao wanafunzi wanaweza kuusikiliza kisha wakaandika hadithi kuhusu wimbo huo. Wanafunzi pia hupewa zoezi la kutayarisha video kuhusu majengo ya shule yao katika lugha ya Kiswahili kisha wakaiweka kwa *YouTube*. Chombo hiki cha teknolojia ni chombo muhimu sana katika kutimiza wajibu wa kunufaisha masomo. Hata hivyo, Snelson (2008) anafafanua kuwa kwa sababu baadhi ya maudhui kwenye *YouTube* hayakidhi mahitaji ya kisomo, inakuwa vigumu kwa mwalimu kuchagua ni sehemu ipi itakidhi malengo ya somo lake.

## **Google Docs**

*Google Docs* ni hati ambazo hupatikana mtandaoni. Mtu yeyote anaweza kuzitumia katika kuandika na kurekebisha kazi ya mtu au watu kadhaa. Jambo la kufahamu ni kuwa katika matumizi ya hati hizi, ambazo huwa katika mifumo ya hati za Microsoft kama vile *Microsoft Word*, *Microsoft Power Point*, *Microsoft Excel*, zinaweza kutazamwa na kurekebishwa na mwalimu. Mfumo huu wa *Google Docs* ni mbinu ya usomaji kwa ushirika. Mwalimu hutumia hati hizi kuboresha uandishi wa wanafunzi wa lugha ya Kiswahili. Mwalimu anaweza kutoa anwani ya hadithi na kuiweka katika hati za *Google Docs* kisha wanafunzi wakatarajiwa kukamilisha hadithi hiyo. Wanafunzi wengi wanaweza kutazama shughuli ya kila mmoja wao. Wana uhuru wa kufuta na kurekebisha tungo zao. Mwalimu pia hupata fursa ya kurekebisha kazi za wanafunzi. Tatizo la aina hii ya teknolojia ni kuwa lazima kuwepo na mtandao.

## **Mitandao ya kijamii – Facebook na Blogu**

Mitandao ya kijamii imatumiwa kuboresha ufundishaji wa lugha ya Kiswahili kupitia mazungumzo na maingiliano baina ya wanafunzi na mwalimu. Kwa mfano, kwa kutumia *Facebook* mwalimu huanzisha kikundi cha somo lake na kuwaalika wanafunzi kwenye kikundi hicho. Kila mwanafunzi hutarajiwa kukubali mwaliko huo. Baada ya kukubali mwaliko, mojawapo ya zoezi la kila wiki hutolewa. Zoezi hili huwa ni kuchapisha angalau chapisho moja au kusasisha hali, kuuliza maswali au hata kusambaza mambo wanayopata kuhusu lugha ya Kiswahili. Baadhi ya mazoezi yaliyotajwa hufanywa katika lugha ya Kiswahili. Wanafunzi hutoa maoni kuhusu chapisho au sasisho la mwenzao. Blogu pia hunufaisha masomo ya Kiswahili. Mwalimu huunda blogu na kuchapisha hadithi au shairi. Wanafunzi hutarajiwa kutoa maoni yao au uhakiki wao kuhusu shairi au hadithi hiyo kwenye blogu iliyoundwa.

## **Mtandao**

Mwalimu hutumia mtandao kuwafanyisha wanafunzi mazoezi ya kusoma, kuandika na kusikiliza. Wanafunzi husikiliza habari za moja kwa moja kama ilivyo katika nchi ya Kenya, Uganda au Tanzania kupitia usambazaji wa moja kwa moja. Wanafunzi hupata fursa ya kusoma magazeti ya Kiswahili kutoka nchi ya Tanzania na Kenya. Mtandao wa *Swahili Hub* hutoa nakala ya kielektroniki ya gazeti la *Taifa Leo*.

## **Video na CD**

Vifaa hivi ni vifaa vya kiteknolojia vya jadi. Ingawa vinachukuliwa kuwa vifaa vya jadi vina nafasi kubwa katika kuboresha ufundishaji wa lugha. Mwalimu hutayarisha video na CD kuhusu utamaduni wa Afrika Mashariki kama vile ndoa za tamaduni za Kiafrika, jando nchini Afrika, uzazi barani Afrika, soko la Afrika na kadhalika. Mwalimu anapofunza sehemu hiyo huonyesha video au huweka CD aliyotayarisha ili wanafunzi waweze kufahamu utamaduni wa jamii inayozungumza lugha inayofundishwa. CD pia hutumiwa kuboresha matamshi. Mwalimu hurekodi sauti za Kiswahili na huwapa wanafunzi CD hiyo ambayo wanatarajiwa kuzitambua sauti hizo.

Vifaa hivi vya teknolojia vinanufaisha mafunzo ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Syracuse huku vikifanya ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili kufurahisha. Lugha ya Kiswahili kwa kweli imenufaika zaidi na teknolojia hii. Ufundishaji wa Kiswahili katika miaka hamsini iliyopita umeathiriwa sana na teknolojia. Maendeleo haya hayapo tu katika nchi za ng'ambo bali pia hata katika Ukanda wa Afrika Mashariki. Hata hivyo, walimu wanaotoka Afrika Mashariki hukumbwa na changamoto katika juhudi zao za kufunza Kiswahili katika vyuo nchini Marekani.

## **Changamoto za ufundishaji wa lugha ya Kiswahili nchini Marekani**

Ufundishaji wa lugha yoyote hasa ile ya pili au ya kigeni hukumbwa na changamoto kadha wa kadha. Kiswahili katika mazingira ya nchi ngeni kimepata changamoto zake. Changamoto hizi bado zingali zinakabiliwa na kuna juhudi zaidi mwaka baada ya mwaka zinazofanywa. Washikadau wana matumaini kwamba sekta ya Kiswahili nchini Marekani itanawiri na kuendelea kupiga hatua. Miongoni mwa changamoto hizi ni idadi ya usajili wa wanafunzi katika somo la lugha ya Kiswahili, mielekeo hasi ya wanafunzi kuhusu lugha za Kiafrika- Kiswahili ikiwemo, ufadhili wa lugha ya Kiswahili

na kubaguliwa kwa lugha za Kiafrika dhidi ya lugha zenye misingi imara kama vile Kifaransa, Kihispania na Kijerumani.

Katika miaka ya 1970 tatizo kubwa kwa lugha za Kiafrika lilikuwa ni *usajili wa lugha hizo katika vyuo vya Marekani*. Temu (1992) anaeleza kuwa Tume ya Rais ya Kuchunguza Hali ya Lugha za Kigeni nchini Marekani ilieleza kuwa tatizo kubwa lililokumba Lugha za Kiafrika lilikuwa usajili mdogo wa wanafunzi. Ripoti ya tume hii ilionyesha kuwa asilimia kumi na tano tu ya wanafunzi wa shule za upili za Marekani ndio walijifunza lugha za Kiafrika. Asilimia hiyo ilikuwa imepunguka kutoka asilimia ishirini na nne mnamo mwaka wa 1965. Idadi hii ikilinganishwa na lugha zenye umaarufu zaidi kama vile Kifaransa, Kihispania na Kijerumani ilikuwa ya chini mno. Katika Chuo Kikuu cha Syracuse, lugha ya Kiswahili imekuwa na wanafunzi wachache wanaojisajili na kulipia masomo ya lugha hiyo ilhali kuna wanafunzi wengi wanaotaka kujifunza Kiswahili bila kulipia. Kwa upande mwingine wanafunzi wenye asili ya Kiafrika huwa wachache zaidi katika kundi la wasiolipia. Kutokana na idadi ndogo ya wanafunzi wanaojisajili, huwa ni vigumu kumfadhili mwalimu wa lugha ya Kiswahili kutoka Afrika Mashariki. Hata hivyo, katika Chuo Kikuu cha Syracuse kuna matumaini kutokana na juhudi za Idara ya Lugha, Fasihi na Isimu kutanguliza somo la Mbinu za Utafiti wa Kiisimu huku ikitafuta data ya kiisimu ya lugha za Kibantu. Hatua hii imewafanya wanafunzi wengi kutaka kujifunza lugha ya Kiswahili.

Tatizo lingine ni kwamba wanafunzi wa nchi ya Marekani mara nyingi huwa hawaoni haja ya kujifunza lugha za Kiafrika. Baadhi ya wanafunzi huona kuwa lugha za Kiafrika hazina nafasi za ajira kama lugha za Ulaya. Wanafunzi wa asili ya Afrika pia huwa ni tatizo. Wanafunzi hawa mara nyingi huona kwamba lugha za Kiafrika hazina umuhimu katika maisha yao. Mwalimu anaweza kutatizika sana na mwanafunzi ambaye alichukua somo la Kiswahili ili kutimiza mahitaji ya shahada ya kwanza kwa sababu mwanafunzi huyo wakati mwingine hana motisha ya kusoma na kuifahamu lugha hii. Wakati mwingine huwa hawatii bidii katika kazi ya ziada na mazoezi. Kwa upande mwingine, mwanafunzi anayesoma lugha ya Kiswahili ili kupata maarifa huwa ana motisha ya kutaka kujua mengi na kuifahamu na hata kuwasiliana kwa kutumia lugha hiyo. Idadi kubwa ya wanafunzi wanaosoma Kiswahili chuoni Syracuse ni wale ambao wanataka kujifahamisha zaidi kuhusu Afrika. Hawa huwa wana motisha na huonyesha juhudi katika masomo ya Kiswahili.

Mwalimu aliye na utamaduni na itikadi tofauti kuhusu masomo hutatizika katika juhudi za kujenga mshawasha miongoni mwa wanafunzi wake. Katika bara la Afrika, mwanafunzi anatarajiwa kujisukuma. Wanafunzi wa nchi ya Marekani mara nyingi husukumwa zaidi. Kwa hivyo, changamoto kubwa ni kuzua mbinu za kila siku za kujenga motisha kwa wanafunzi. Wanafunzi wa shahada ya uzamili na uzamifu katika Chuo Kikuu cha Syracuse wana motisha zaidi. Wanafunzi hawa wanapojiunga na masomo ya lugha ya Kiswahili wale wa shahada ya chini wanadumisha viwang'ô vya wanafunzi hawa.

Swala la kubaguliwa kwa lugha za Kiswahili haliwezi kuepukika. Lugha zenye zinazotambulika zaidi hupewa nafasi kubwa katika vyuo vingi. Lugha hizi hujumuisha Kifaransa, Kichina, Kijapani, Kihispania na Kijerumani. Idara nyingi za lugha zinapojipata na lugha ndogo ndogo kama vile Kiswahili huwa hazitilii maanani sana lugha hizi. Katika vyuo vingine Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika hushirikishwa katika Idara za Masomo ya Kiafrika. Kutokana na juhudi hizi lugha za Kiafrika hupata wapenzi na washikadau ambao huandaa na kutayarisha kongamano na semina za kuwaleta wapenzi wa Kiswahili katika chuo kuja kuboresha matamshi yao. Katika Chuo Kikuu cha Syracuse, Idara ya Masomo ya Kiafrika imekuwa katika harakati za kutaka kuhamisha Kiswahili kutoka Idara ya Lugha, Fasihi na Isimu hadi idara hiyo ili iweze kushughulikia lugha ya Kiswahili kikamilifu.

Tatizo kuu ni lile la ufadhili wa lugha ya Kiswahili. Bila ufadhili wa lugha hii ni vigumu mno kuifunza. Ufadhili hujumuisha gharama ya masomo ya mwalimu na pesa za matumizi za mwalimu huyo. Ufadhili wa programu za lugha ya Kiswahili umethiriwa na mfumuko wa uchumi ulimwenguni. Chuo Kikuu cha Syracuse kimeathiriwa na tatizo hili na kwa sasa hakuna ufadhili wa lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo, lugha hii haifundishwi katika Chuo hiki mwaka wa 2013/2014. Hata hivyo, hali ya kijumla ya ufadhili wa lugha za Kiafrika imeanza kupata matumaini zaidi. Baadhi ya mashirika kama vile Shirika la *National Science Foundation* limeendelea kutoa ufadhili wake kwa utafiti wa lugha za Kiafrika. Miaka michache ijayo lugha ya Kiswahili itapata kuendelea, kukua na kufadhiliwa zaidi.

## **Mapendekezo na Hitimisho**

Katika kuadhimisha miaka 50 ya Kiswahili ni muhimu kutambua kuwa washikadau wa Kiswahili Barani Afrika na ng'ambo wana umuhimu katika

kueneza Kiswahili kimataifa. Jukumu la kuendeleza lugha ya Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika katika nchi za ng'ambo limeachiwa serikali, vyuo na washikadau wa lugha hizo katika nchi hizo. Lakini washikadau wa lugha ya Kiswahili barani wana nafasi kubwa ya kuboresha hali ya Kiswahili ulimwenguni.

Vyuo vya nchi za Afrika Mashariki vinaweza kuandaa mikataba na vyuo vya nchi za ng'ambo ya kusaidia wanafunzi kuja katika nchi hizi na kujizamisha katika masomo ya Kiswahili kwa angalau mwaka mmoja. Mikataba hii itajumuisha makazi ya wanafunzi hawa na namna ya kuhamisha gredi watakazopata katika vyuo vya Afrika Mashariki hadi vyuo vyao. Miradi hii ipo katika Chuo Kikuu cha Kenyatta lakini ipo haja ya vyuo vyote kuungana na kuwa na sauti moja katika kutafuta nafasi hizi.

Walimu na wanafunzi katika masomo ya Kiswahili wana nafasi ya kuandika mapendekezo ya ufadhili wa miradi maalumu ya kuitangaza lugha ya Kiswahili na utamaduni wake. Miradi hii inaweza kuandikiwa mashirika kama vile *The National Science Foundation* na Shirika la UNESCO ili kutafuta ufadhili wa lugha ya Kiswahili. Ufadhili huu utajikita katika kutafiti maswala ya kitamaduni ya lugha na pia kuunda nafasi za wanafunzi wa ng'ambo kuja Afrika Mashariki. Pia mapendekezo ya miswada ya kuwapeleka wanafunzi wa Kiswahili katika nchi za ng'ambo kusoma na kufundisha Kiswahili ni jukumu la vyuo.

Washikadau wa Kiswahili wanaweza kuungana na mashirika ya utalii Afrika Mashariki katika kutoa matangazo ya kusifu lugha ya Kiswahili na kuonyesha umuhimu wake. Baadhi ya matangazo ya mashirika haya yaweza kutumia nyimbo za Kiswahili lakini yasikomee hapo, bali pia yaendelee kutoa mafunzo kuhusu lugha ya Kiswahili. Mafunzo haya yanaweza kutolewa wakati wa maonyesho ya kimataifa ya utalii nchini Marekani. Washikadau pia lazima wahimize serikali za Kenya, Uganda na Tanzania kuipa lugha ya Kiswahili hadhi kubwa katika masuala ya kitaifa na kimataifa. Hali hii itasaidia baadhi ya wanafunzi kuona umuhimu wa lugha ya Kiswahili Afrika Mashariki na kuisoma.

Katika miaka 50 ya ufundishaji wa Kiswahili imedhihirika kuwa taaluma ya ufundishaji wa Kiswahili inaendelea kukua na kupata umaarufu katika nchi za kigeni. Lugha ya Kiswahili inaendelea kupata wanafunzi na kwa sasa itaendelea kukua katika nchi za ng'ambo. Kila mmoja wetu ana jukumu la kuinua hadhi ya lugha ya Kiswahili. Teknolojia ya kisasa inatoa nafasi kubwa kwa Kiswahili kunufaika nayo. Matumizi ya Kiswahili katika vifaa

vya kiteknolojia itawezesha lugha ya Kiswahili kunawiri zaidi na kuendelea kupata wanafunzi wengi. Ni muhimu kufahamu kuwa lugha ya Kiswahili ingali changa, na ikiwa katika miaka hamsini imepata maendeleo ya kiwango cha juu, basi kuna matarajio kwamba lugha hii itaendelea kupata maendeleo zaidi. Changamoto kwa washikadau na wapenzi wa lugha ya Kiswahili barani Afrika zipo sio tu katika kuachia nchi za ng'ambo kukuza lugha ya Kiswahili huko ng'ambo lakini pia kushiriki katika kukuza lugha ya Kiswahili kitaifa na kimataifa.

## **Marejeleo**

- Blake, R. (2008). *Brave New Digital Classroom: Technology and Foreign Language Learning*. Washington, D.C: Georgetown UP.
- Bokamba, G. (2000). *African Languages Program Development and Administration. A History and Guidelines for Future Programs*. NALRIC, University of Wisconsin, Madison.
- Bokamba, G and Mchombo, S. (2009). Review Report of the National African Language Resource Center (NALRC) at the University of Wisconsin-Madison.
- Cetto, M (2011). Technology and Second Language Teaching. University of California, Davis.
- Hoopingarner, D (2009). "Best Practices in Technology and Language Teaching." *Language and Linguistics Compass* 3.1, 222-233.
- Moshi, L. (2011). "A Transformation of African Language Teaching in the United States: The Emergence of a Filed Superstructure." Katika *Selected Proceedings of the 40<sup>th</sup> Annual Conference on African Linguistics* 26-35. Bokamba, G et al. Somerville M.A. Cascadilla Proceeding Project.
- Mugane, J. (1997). "Learning African Languages with evolving Digital Techonology." *African Learning*.
- Snelson, C. (2008). "Web-Based Video in Education: Possibilities and Pitfalls." *TCC 2008 Proceedings*.
- Temu, N. (1992). "African -American Students' Self Awareness through Kiswahili Language." *Journal of Black Studies*.
- Wiley, D. (2008). Priorities for U.S Instruction in the African Languages: New Criteria and New Choices. *E-LCTL Initiative: A National Project for U.S EDVI Programs, National Planning for the Teaching of less Commonly Taught Languages*.